## HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO

## MUHTASARI WA KIKAO MAALUM CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 20/01/2022 KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA

### WAJUMBE WALIOHUDHURIA:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 01: | Diwani M. A. Usinga | - | Mwenyekiti |
| 02: | Diwani C.D. Chandika | - | Makamu Mwenyekiti |
| 03: | Mh. Muharami Mkenge (MB) | - | Mjumbe |
| 04: | Diwani A. A. Issa | - | Mjumbe |
| 05: | Diwani S. A. Ngatipura | - | Mjumbe |
| 06: | Diwani A.M. Pyalla | - | Mjumbe |
| 07: | Diwani S. R. Honello | - | Mjumbe |
| 08: | Diwani U.M. Kisebengo | - | Mjumbe |
| 07: | Ndg.Selenda, Shauri | - | M/Mtendaji (W) – Katibu |

### WATAALAM WALIOHUDHURIA:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 01: | Ndg. Kapinga, M.M. | - | Afisa Mipango (W) |
| 02: | Ndg. Mwalukasa,G.A. | - | Afisa Utumishi/Utawala (W) |
| 03: | Adv. Malogo, H. | - | Mwanasheria H/Wilaya |
| 04: | Ndg. Shindai, P.M. | - | Mkaguzi wa Ndani (W) |
| 05: | Ndg. Mhina, M.S. | - | Mkuu wa Kitengo cha Misitu/Nyuki |
| 06: | Ndg. Kissimbo, M. | - | Afisa Kilimo/Umwagiliaji (W) |
| 07: | Ndg. Maleko, D. | - | Afisa M/Jamii (W) |
| 08: | Ndg. Stili, A. | - | Afisa Mtendaji Mkuu M/Mji |
| 09: | Ndg. Nteye, A.S | - | Afisa Ugavi na Manunuzi (W) |
| 10: | Dr. Israeli, N. | - | Afisa Hifadhi ya Mazingira |
| 11: | Ndg. Kaziyareli, A | - | Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 12: | Ndg. Ruth Barnabas | - | Kaimu Mweka Hazina (W) |
| 13: | Ndg. Mpemba. A | - | Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W) |
| 14: | Ndg. Guzuye, B. | - | Kaimu Afisa TEHAMA |
| 15: | Ndg. Kajigili, W. | - | Kaimu Afisa Elimu Msingi (W) |
| 16: | Eng. Martine, W. | - | Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W) |
| 17: | Dr. Mwakipesile, L. | - | Kaimu Mganga Mkuu (W) |
| 18: | Ndg. Luhamba, A. | - | Kaimu Mratibu wa TASAF H/W |

*KATIBU:............................*  *M/KITI:...........................*

**WATAALAM WASIOHUDHURIA:**

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 01: | Ndg. Izina, W. | - | AG. DLNRO | - | Kwa taarifa |
| 09: | Ndg. Urassa, T. | - | EO | - | Kwa taarifa |

**SEKRETARIETI:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 01: | Ndg. Semkuya, B.E. | - | CC |
| 02: | Ndg.Katikiro, P.M. | - | CC |

**MUHT.NA.HWB/FUM/10/143/2021/2022 - KUFUNGUA KIKAO**

Mkurugenzi Mtendaji (W) ambaye pia ni Katibu wa Kikao hiki alianza kwa kuwafahamisha Wajumbe kwamba, Kikao hicho kilikuwa ni Kikao maalum cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kwa ajili ya kupokea na kujadili Agenda maalum kama zilivyoandaliwa kutoka Idara ya Mipango na Idara ya Afya kwa ajili ya kutolewa maamuzi kwa hatua za utekelezaji kutokana na umuhimu wake

Baada ya Katibu kutoa maelezo hayo ya utangulizi alimkaribisha Mwenyekiti kufungua Kikao hicho.

Mwenyekiti aliwakaribisha Wajumbe wote waliohudhuria katika Kikao hicho, aidha aliwasihi kushirikiana kikamilifu katika kujadili taarifa hizi maalum kama zilivyoandaliwa ili hatimaye kuweza kutoa maoni na ushauri kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa shughuli zilizobainishwa kwa lengo la kuboresha na kuleta ufanisi katika utekelezai wa shughuli mbalimbali katika H/Wilaya Bagamoyo.

Mwenyekiti alikifungua Kikao saa 08.20 mchana.

**MUHT.NA.HWB/FUM/10/144/2021/2022 - KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 20/01/2022**

Kikao kiliwasilishiwa na kusomewa Agenda za Kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 20/01/2022 kama ifuatavyo: -

01: Kufungua Kikao

02: Kuthibitisha Agenda za Kikao maalum cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 20/01/2022

03: Maombi ya kibali cha ujenzi wa jengo la Huduma za dharua (EMD) katika Hospitali ya (W) Bagamoyo na ujenzi wa jengo la nyumba ya Watumishi (3 in 1) katika Kituo cha Afya Fukayosi kwa kutumia utaratibu wa **"Force Account"** na matumizi ya Tshs. 3,000,000/= kwa ajili ya Usimamizi wa miradi kutoka mapato ya ndani

04: Kuwasilisha gharama kwa ajili ya ubomoaji wa jengo la Ofisi za Utawala za Hospitali ya Wilaya kupisha Mradi wa ujenzi wa jengo la Huduma za Dharura (EMD)

05: Maombi ya Kibali cha kufanya Mabadiliko ya fedha Tshs. 93,200,000/= kutoka Mradi wa Kituo cha Afya Fukayosi kwenda kwenye ujenzi wa vyoo katika Shule Shikizi za Msingi

06: Mabadiliko ya aina ya bati zitakazoezekwa katika Kituo cha Afya Fukayosi

07: Taarifa ya kuanzisha Vitalu vya Miche ya Korosho kwa Mkataba Msimu wa mwaka 2021/2022

08: Kufunga Kikao

Wajumbe walizipokea Agenda hizo, kisha kwa pamoja walizipitisha kuwa ni Agenda sahihi kwa ajili ya kujadiliwa katika Kikao maalum cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 20/01/2022 kama zilivyowasilishwa.

**MUHT.NA.HWB/FUM/10/145/2021/2022 - MAOMBI YA KIBALI CHA UJENZI WA MRADI WA JENGO LA HUDUMA ZA DHARURA NYUMBA YA WATUMISHI WA KITUO CHA AFYA FUKAYOSI KWA KUTUMIA "FORCE ACCOUNT" NA MATUMIZI YA TSHS. 3,000,000/= KWA AJILI YA USIMAMIZI WA MIRADI KUTOKA MAPATO YA NDANI**

Kikao kiliwasilishiwa na kusomewa taarifa kuhusiana na maombi ya ujenzi wa mradi wa jengo la Huduma za Dharura (EMD) na Nyumba ya Watumishi katika Kituo cha Afya Fukayosi kwa kutumia "Force Account". Muhtasari wa maelezo ni kama ifuatavyo:-

*KATIBU:............................* *M/KITI:...........................*

**Muhtasari wa maelezo:**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) ilipokea fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO – 19 ambapo jumla ya Tshs. 300,000,000/= za ujenzi wa jengo la Huduma za Dharura (EMD) katika Hospitali ya Wilaya na Tshs. 90,000,000/= ujenzi wa nyumba ya Watumishi (3 in 1) katika Kituo cha Afya Fukayosi zilipokelewa.

Fedha hizi zililetwa na maelekezo kwamba, ujenzi wa miradi hii yote miwili itekelezwe kwa kutumia Wakandarasi ambao wangepatikana kwa kutumia taratibu za manunuzi.

Katika hatua za kutekeleza maelekezo hayo ya Serikali, Tangazo la Zabuni lilitolewa katika gazeti la Habari leo la tarehe 18/12/2021. Waombaji waliojitokeza na gharama walizoomba ni kama ifuatavyo:-

| A: JENGO LA HUDUMA ZA DHARURA - EMD | | | |
|---|---|---|---|
| **NA** | **JINA LA KAMPUNI** | **GHARAMA** | **MUDA** |
| 1 | MC Elack Investment Co. Ltd,<br>S.L.P. 10131,<br>**DAR ES SALAAM** | 796,278,692.00 | Miezi 4 |
| 2 | Kuyella Enterprises, Ltd.,<br>S.L.P. 2880,<br>**DAR ES SALAAM** | 554,752,190.00 | Siku 140 |

| B: JENGO LA HUDUMA ZA DHARURA - EMD | | | |
|---|---|---|---|
| **NA** | **JINA LA KAMPUNI** | **GHARAMA** | **MUDA** |
| 1 | CAF investment Ltd,<br>S.L.P. 1490,<br>**DAR ES SALAAM** | 273,039,226.00 | Miezi 4 |
| 2 | Kuyella Enterprises, Ltd.,<br>S.L.P. 2880,<br>**DAR ES SALAAM** | 149,889,302.00 | Siku 91 |
| 3 | Kisano (2007) Tanzania Ltd.<br>S.L.P. 70567,<br>**DAR ES SALAAM** | 224,176,801.20 | Miezi 4 |

Baada ya kufunguliwa kwa Zabuni hizo ilionekana kwamba gharama zilizoombwa na Wakandarasi zilikuwa kubwa sana ambapo taarifa ya kukosekana kwa Wakandarasi ambao gharama zao zinalingana na Bajeti iliyopo iliwasilishwa kwa Katibu Tawala Mkoa wa Pwani

Hata hivyo Katibu Tawala Mkoa wa Pwani aliwasilisha taarifa hizo kwa Katibu OR - Mkuu TAMISEMI, ambapo Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) ilipokea barua yenye Kumb. Na.AH.161/198/01 ya tarehe 14/01/2022 kutoka kwa Katibu Tawala Mkoa wa Pwani ikiwa na maelekezo kwamba miradi ya ujenzi wa jengo la huduma za dharuza (EMD) katika Hospitali ya Wilaya Bagamoyo na mradi wa ujenzi wa nyumba ya watumishi (3 in 1) katika Kituo cha Afya Fukayosi itekelezwe kwa kutumia utaratibu ,wa "Force Account" hii ni kutokana na changamoto zilizojitokeza za upatikanaji wa Wakandarasi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii kwa nchi nzima.

Aidha kwa kuwa miradi hii ya ujenzi wa nyumba ya Watumishi Fukayosi na ujenzi wa jengo la Huduma za dharura (EMD) haina fedha za usiamamizi, ofisi ya Mganga Mkuu Wilaya inapendekeza itolewe idhini ya matumizi ya Tshs. 3,000,000/= kutoka mapato ya ndani au fedha za miradi ya maendeleo za mapato ya ndani kwa ajili ya usimamizi wa miradi hiyo hususani ni kwa ajili ya ununuzi wa mafuta, shajala n.k.

Baada ya Wajumbe kupokea muhtasari huo wa maelezo, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) iliwasilisha maombi ya Kibali cha ujenzi wa miradi ya jengo la Huduma za Dharura katika Hospitali ya Wilaya Bagamoyo na ujenzi wa Mradi wa Nyumba ya Watumishi (3 in 1) katika Kituo cha Afya Fukayosi kutekelezwa kwa kutumia utaratibu wa "Force Account" ambapo:-

(a) Kamati tatu (3) za utekelezaji wa miradi kwa utaratibu wa "Force Account" zitaundwa kama ifuatavyo:-

  (i) Kamati ya Ujenzi
  (ii) Kamati ya Manunuzi
  (iii) Kamati ya Mapokezi

(b) Taraibu za kupata mafundi zitaendelea baada ya kupata mchanganuo wa kazi **(Schedule of Labour)** toka ofisi ya Mhandisi wa Ujenzi Wilaya

(c) Utayarishaji wa michanganuo wa vifaa **(Schedule of Materials)** unaendelea kwa kutumia ofisi ya Mhandisi wa Ujenzi Wilaya

*KATIBU:............................* *M/KITI:............................*

Kikao kiliipokea taarifa hiyo, kisha Wajumbe waliijadili kwa kina, katika kuijadili taarifa hiyo, Wajumbe walieleza kuwa hawana pingamizi kuhusiana na kuridhia maombi ya mradi wa ujenzi wa jengo la Huduma za Dharua (EMD) katika Hospitali ya Wilaya Bagamoyo na Mradi ujenzi wa Nyumba ya Watumishi katika Kituo cha Afya Fukayosi kutekelezwa kwa kutumia mfumo wa "Force Account".

Hii ni kwa kuzingatia kuwa, maelekezo yaliyotolewa na Serikali ya kutumia Wakandarasi yameshindikana kutokana na changamoto ya kukosa Wakandarasi ambapo hatua muhimu za kutoa taarifa kuanzia ngazi ya Mkoa hadi OR - TAMISEMI zimetekelezwa. Kwa lengo la kutokwamisha utekelezaji wa miradi hii muhimu kwa Wananchi wa Bagamoyo.

Aidha kuhusu hoja ya kuridhia kibali cha matumizi ya fedha za mapato ya ndani kiasi cha Tshs. 3,000,000/= kutoka kwenye mapato ya ndani kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa utekelezaji wa mradi, ni ya msingi na hasa kwa kuzingatia shughuli za utekelezaji wa mradi zinahitaji usimamizi na ufuatiliaji wa karibu kwa kila siku. Wajumbe wote kwa pamoja walifikia makubaliano kuwa;

**MAKUBALIANO:**

01: Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wote kwa pamoja ***Waliridhia*** kibali cha utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa jengo la Huduma za dharua (EMD) katika Hospitali ya Wilaya Bagamoyo wenye thamani ya Tshs. 300,000,000/= na Mradi ujenzi wa Nyumba ya Watumishi (3 in 1) katika Kituo cha Afya Fukayosi wenye thamani ya Tshs. 90,000,000/= kutekelezwa kwa kutumia utaratibu wa **"Force Account"** kama ilivyowasilishwa sambamba na kuwasilishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani ujao

02: Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wote kwa pamoja **Waliridhia** kibali cha matumizi ya fedha za mapato ya ndani Tshs. 3,000,000/= kutoka vifungu vya Idara ya Afya kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa utelelezaji wa mradi kama ilivyowasilishwa sambamba na kuwasilishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani ujao

*KATIBU:..............................* *M/KITI:............................*

**MAKUBALIANO:**

01: Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wote kwa pamoja ***Walidhia*** Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo kuanzisha Kitalu cha Miche ya Korosho kwa Mkataba katika kipindi cha msimu wa mwaka 2021/2022

02: Taarifa kuhusu Halmashauri ya Wilaya kuanzisha Vitalu vya Miche ya Korosho katika Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo kwa Mkataba katika kipindi cha msimu wa mwaka 2021/2022 iwasilishwe kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani ujao

**MUHT.NA.HWB/FUM/10/150/2021/2022 - KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru Wataalam kwa michango yao waliyoitoa na hatimaye kufanikisha Kikao hicho maalum kwa lengo la kuwezesha Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi husika kwa wakati.

Aidha alisisitiza Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) kuelekeza fedha za miradi ya maendeleo pindi zinapopokelewa kwenye maeneo ya miradi kwa wakati kwa lengo la kuwezesha kukamilisha miradi kwa wakati na hatimaye miradi yote inayotekelezwa kuweza kutoa huduma kwa jamii na hivyo kuweza kufikia malengo ya Serikali Kuu na Halmashauri ya Wilaya kwa uumla wake.

Mwenyekiti alikifunga Kikao mnamo saa 09.50 Alaasiri.

**U M E T H I B I T I S H W A**

| | |
|---|---|
| ......................................... | ......................................... |
| *Shauri, Selenda* | *Mohamed A. Usinga* |
| **MKURUGENZI MTENDAJI (W)** | **MWENYEKITI** |
| **KATIBU** | **HALMAHAURI YA (W)** |

**TAREHE** 22/02/2022